



WIZARA YA ELIMU,  
SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# MoEST Weekly

17 Aprili, 2026



**TUZO YA TAIFA YA MWALIMU  
NYERERE KUIMARISHA UANDISHI  
BUNIFU**

## SERIKALI YAIMARISHA TUZO YA TAIFA YA MWALIMU NYERERE YA UANDISHI BUNIFU

**S**erikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuwekeza katika Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere, hatua inayolenga kuhamasisha ubunifu, kukuza fasihi ya Kiswahili na kuendeleza utamaduni wa kusoma na kuandika nchini.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema kuwa Serikali imeendelea kuthamini na kuenzi mchango wa Baba wa Taifa, Hayati Julius Kambarage Nyerere katika fasihi na uandishi bunifu kwa kuanzisha na kuendeleza tuzo hiyo yenye hadhi ya kitaifa na kusisitiza kuwa lengo ni kuendeleza urithi wake na kuhamasisha kizazi kipya.

Akizungumza Aprili 13, 2026 katika hafla ya utoaji wa tuzo hizo, Prof. Mkenda ameeleza kuwa Mwalimu Nyerere hakuwa tu kiongozi wa kisiasa bali pia mtunzi mahiri wa fasihi aliyetoa mchango mkubwa katika kukuza lugha utamaduni wa Kiswahili. Ameongeza kuwa tuzo hizo zinahamasisha vijana na wanafunzi kujitakatika uandishi na ubunifu.

Aidha, Prof. Mkenda amemshukuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuidhinisha matumizi ya jina la Mwalimu Nyerere katika tuzo hizo, akibainisha kuwa hatua hiyo inaendeleza historia na kuimarisha thamani ya taaluma ya uandishi bunifu nchini.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo, amesema Serikali imetenga shilingi bilioni 4.2 katika kipindi cha miaka minne tangu kuanzishwa kwa tuzo hiyo kwa ajili ya uendeshaji, uchapishaji wa vitabu na utoaji wa zawadi kwa washindi. Amesema uwekezaji huo umeongeza ari ya waandishi na kuimarisha sekta ya uchapishaji.



**Mwl. Abdilatif Abdalla**  
Mwandishi Nguli wa Vitabu



**Prof. Adolf Mkenda**  
Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia





Prof. Nombo ameongeza kuwa Wizara inapanga kushirikiana na vyuo vikuu na idara za fasihi kuendesha warsha kwa waandishi chipukizi pamoja na kongamano la kitaifa la uandishi bunifu ili kuongeza hamasa ya uandishi. Pia ametoa wito kwa Watanzania kuendeleza utamaduni wa kusoma na kuandika vitabu.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Dkt. Anneth Komba, amesema uandishi bunifu ni nyenzo muhimu ya kufanikisha malengo ya elimu, akieleza kuwa sera inalenga kukuza stadi za kusoma, kuandika na kuwasiliana kwa Kiswahili pamoja na kujenga fikra makini kwa wanafunzi.

Kwa upande wake, mwandishi nguli Mwl. Abdilatif Abdalla amesema uandishi bunifu si anasa bali ni nyenzo ya kujenga fikra, kuelewana kuibadilishajamii, huku akisisitiza umuhimu wa kuendeleza utamaduni wa kusoma na kuandika ili kukuza maarifa na maendeleo ya kijamii.



**Prof. Carolyne Nombo**  
Katibu Mkuu



**Dkt. Anneth Komba**  
Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET)